



Taarifa kuhusu Kutangazwa Mwenyeheri kwa Sista Maria Carola latolewa katika Mkeshwa wa Jubilei ya miaka 50 ya uwepo wa Cottolengo nchini Kenya

Mama Mkuu wa Masista wa Cottolengo, **Sista Elda Pezzuto**, Pamoja na Baba Mkuu wa Chumba Kidogo, **Padre Carmine Arice**, na Mkuu wa Mabrua wa Cottolengo, **Bruda Giuseppe Visconti**, wakati kwa sasa wapo nchini Kenya kwa ajili ya maadhimisho Jubilei ya miaka 50 tangu kurejea kwa Familia ya Cottolengo barani Afrika, wanapokea kwa furaha kubwa taarifa kwamba Baba Mtakatifu Francis ametoa kibali cha kuadhimisha ibada ya Kutangaza Mwenyeheri Mtumishi wa Mungu Sista Maria Carola Cecchin (1877-1925), wa Shirika la Masista wa Mtakatifu Joseph Cottolengo, Jumamosi, **Novemba 5, 2022** huko **Meru, Kenya**.

Sherehe hizo zitaongozwa na **Mwadhama Kardinali John Njue**, Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu la Nairobi, ambaye atawakilisha Kiongozi Mkuu wa Kanisa Katoliki.

Wakuu wa Familia ya Cottolengo, iliyoenea duniani kote, na hasa kwenye ardhi ya Afrika, wanatoa shukrani kwa Baba Mtakatifu kwa kutoa nafasi ya kusherehekea kutangazwa Mwenyeheri kwa Sista Maria Carola katika nchi ambayo aliyopenda sana. "Inashangaza na kufurahisha sana", wanasisitiza, "wema wa Mungu Mpaji, anayetoa habari hii njema haswa katika mkeshwa wa maadhimisho ya Jubilei ya miaka 50 ya uwepo wa Cottolengo Nchini Kenya".

"Ni neema ya pekee", **Padre Arice** anasisitiza, "kwamba Mungu Mpaji anatoa kwa Familia nzima ya Cottolengo iliyopo Afrika na ulimwenguni kama wito mpya kwa njia ya utakatifu".

Mama Pezzuto, Padri Arice na Bruda Visconti, waliopo sasa nchini Kenya, wanaungana nao Masista Jumbe la Afrika na furaha ya familia ya mtoto Msafiri Hilary Kiama aliyepokea muujiza huo kupitia maombezi ya Mstahili-heshima Sista Maria Carola.

Turin (Italia) na Tuuru (Kenya), 11 Machi 2022

Suor Lucia Mossucca - Stefano Di Lullo

www.cottolengo.org

Via Cottolengo, 12 - 10152 Torino, cell. +39 345 6216561

ufficiostampacottolengo@cottolengo.org